

Hadithi

za

Esopo

Kiliandikwa na Esopo
Mtumwa wa Ugiriki wa Kale,
Takriban mwaka 600 kk

Kilitafsiriwa na
Edward Steere
Zanzibar, Mwaka 1880

HADITHI ZA ESOPO.

1. 2.

CHUO CHA KWANZA

1. 2.

CHA KUSOMEA.

1. 2. 3.

1. 2. 3.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA



1.
ZANZIBAR, 1880.

291. g . 50 .

FAHIRISI.

<i>Kijana na mbwa wa mwitu</i>	1
<i>Vijana na vyura</i>	1
<i>Mtu na nyani</i>	2
<i>Sungura na mazabibu</i>	2
<i>Inzi na noondo</i>	3
<i>Mtoto na kijito</i>	3
<i>Panya na paka</i>	4
<i>Simba katika mwitu</i>	4
<i>Kilio cha nguuwe</i>	5
<i>Frasi na punda</i>	6
<i>Njiwa na panya</i>	7
<i>Jogoo na almasi</i>	7
<i>Mfuko wa fetha</i>	8
<i>Mbwa wa mwitu na mwana kondoo</i> ...	9
<i>Imbu na ng'ombe</i>	9
<i>Mwana mbuzi na mbwa wa mwitu</i>	9
<i>Paka asiye na mkia</i>	10

<i>Mwembe na 'mwanzo</i> ...	11
<i>Vyura na mafahali</i> ...	11
<i>Mbwaa wa mwitu samawati</i> ...	12
<i>Mtu na kijana na panda</i> ...	13
<i>Mtu na pesa</i> ...	14
<i>Kuku na mafuranga</i> ...	15
<i>Udongo na waridi</i> ...	15
<i>Mbwaa wa mwitu na korongo</i> ...	15
<i>Punda na chumvi</i> ...	61
<i>Mbwaa wa mwitu na mbwa wa injini</i> ...	16
<i>Mtu na simba na sungura</i> ...	17
<i>Mkulima na pau</i> ...	18
<i>Kunguru na sungura</i> ...	18
<i>Panya na paka na jogoo</i> ...	19
<i>Msufi</i> ...	20
<i>Mbwaa uliyesongwa</i> ...	20
<i>Ndege na nyama na popo</i> ...	21
<i>Tumbili na chupa</i> ...	21
<i>Frasi na mbwa wa mwitu na sungura</i> ...	22
<i>Ndege na makinda yake</i> ...	23
<i>Mtu na samaki</i> ...	23
<i>Ng'ombe na ndama</i> ...	24
<i>Mbwaa wa mwitu na kondoo</i> ...	24
<i>Mwana mbuzi na mbwa wa mwitu</i> ...	25
<i>Jogoo na sungura na mtego</i> ...	25

<i>Mbwa wa mwitu katika ngozi ya kondoo...</i>	26
<i>Bibi na viju kazi vyake ...</i>	26
<i>Nyuki na konokono ...</i>	27
<i>Mzee na mauti</i>	27
<i>Shoka na miti</i>	28
<i>Mbuzi katiku ubao...</i>	28
<i>Punda na kondoo</i>	29
<i>Sungura katika kisima</i>	29
<i>Paa katika majani</i>	30
<i>Sungura na korongo</i>	30
<i>Bata aliyezaa thahabu</i>	31
<i>Mbwa na jogoo na paka</i>	32
<i>Mbwa katika majani...</i>	32
<i>Kuruka katika Rodi</i>	32
<i>Mzee na mtabibu</i>	33
<i>Mbwa na mwivi</i>	34
<i>Yaya na mbwa wa mwitu...</i>	34
<i>Frasi na nyati</i>	35
<i>Kathi na masikini</i>	35
<i>Sungura na paka</i>	36
<i>Upepo na jua</i>	36
<i>Sungura na mbuzi</i>	37
<i>Korongo na mbwa wa mwitu</i>	37
<i>Jogoo na sungura</i>	38
<i>Njiwa na chungu</i>	39

ESOPO.

ESOPO alikuwa mtu Myonani aliyezaliwa kama miaka mia tanu mbele ya Bwana wetu Masiya. Alikuwa mtumwa, na kama walivosema mwenyi kigongo, lakini akili zake nyingi, akakusanya akafanya hadithi nyingi apate kuwafundisha watu kwa mifano.

KIJANA NA MBWA WA MWITU.

KIJANA mmoja aliyechunga kondoo akasi-kiwa dayima kulia, "Mbwa wa mwitu! mbwa wa mwitu!" kwa mchezo tu. Marra mengi, kwa mambo hayo, akawatoa watu kazini kwao koondeni. Walakini walipouona mzaha tu, wakafanya shauri miyoni nwaó kama akilia tena, "mbwa wa mwitu," wasitoke kumsayidia. Mwisho akaja mbwa wa mwitu. Katika wega wake kijana yule akalia sana, "mbwa wa mwitu! mbwa wa mwitu!" lakini sasa hapana mtu kusikiliza sauti yake, mbwa wa mwitu akamua kijana apate kuwala kondoo zake.

VIJANA NA VYURA.

WALIKUWA watoto wakicheza kando la ziwa. Mchezo wao ndio kutupa mawe majini, hivyo wakaumiza sana vyura viliomo ziwanii.

Mwisho chura mmoja, hodari kuliko wenzake, akainua kitwa chake ziwani akasema, "Ee wangwana rafiki zangu, acheni, nakusihii, kwani mchezo wenu ni mauti yetu."

MTU NA NYANI.

MTU aliokaa mashenzini akafuga nyani. Na nyani yule ndio fayida yake, kuweza kufukuza ndege katika matunda na baazi zake. Siku moja mtu yule akalala usingizi wa mchana, yule nyani akakaa ubavuni mwake, akafukuza inzi usoni pake, inzi moja akaja akasimama mwisho wa pua yake. Bassi nyani akacheka, akamfukuza. Tena akaja kidefuni mwake, batta nyani akakasirika sana, akatupa jiwe akampiga inzi, lakini akalitupa kwa nguvu sana hatta akamvunja taya bwana wake.

SUNGURA NA MAZABIBU.

HAPO kale sungura aliona mazabibu mema katika ukuta, akaruka juu asiyapate, akaruka tena kwa nguvu, lakini hakuweza kuyafika, killa arukapo akapungua. Mazabibu yakata-

ndika huko mazuri na mabivu, wala hakuweza kuyapata. Halafu akiona kama haiyamkini kuyafikia, akasema, "Siyataki, mabichi tu."

INZI NA NOONDO.

INZI alikuwa akisimama ukingoni mwa mtungi wa asali, akiona asali tamu akashuka akashuka hatta akashikwa na asali, wala hakuweza kutoka. Noondo akaruka karibu akamkaripia akamwambia, "Huna akili wee, miguu yako na mabawa yako yakufae nini katika asali ?" Baadaye noondo akaona taa katika chumba waliomo, akaruka karibu na karibu hatta akaingia katika moto akafa. Akasema inzi, "Je ? Gissi gani wewe uliyenikaripia kwa sababu ya kupenda asali, umeingia motoni mwenyewe ?"

MTOTO NA KIJITO.

MZEE, aliyemwona mtoto akisimama kando la kijito, akamwuliza, "Mwanangu mbona unakitazama hivi kijito ?" Mtoto akamwambia, "Nangoja hapa, bwana, hatta kijito kitakapo-kwisha kupita, nivuke pakavu." Mzee aka-

mwambia, "Capokubaki kuna nigitu majini. bataenka hatta kufa."

PANYA NA PAKA.

HAPO kale panya walikuwa wakiinwogopa paka, batte hawakuthubuto kutoka, wala mchana wala usiku, asiwaue. Wakaona kama wanakuwa kwa njaa, wakakutana wafanye shauri. Walipokuwa wakiona shaka sana kijana mmoja akaondoka akasemo, "Nimeona shauri jema, ndilo kumfungia paka kengele shingoni tupate kumsikia killa aendako." Panya wakafurahi, wakamsifu sana. Hatta inzee mmoja aliyekuwa amenyamaa kimya, akaondoka akanena, "Shauri hilo ndilo jema, tukiwa na mtu wa kumfungia paka kengele, lakini panya gani athubutuye kumkaribia?"

SIMBA KATIKA MWITU.

WATU wawili walikuwa wakiingia katika mwita msitu, mmoja wao akamwambia mwenziwe, "Tukikota nyama nkali, nitakusayidia wewe, nawe unifanyie hivi." Rafiki yake aka-mwambia, "Vema." Hawajaenda sana alipotoka marru simba katika mwitu. Mtu aliyeetua

shauri njema, akapanda mtini ~~gufche~~. Mwenzake akaogopa sana, wala hakuona bila ya kujiponya illa kuanguka chini na kuizua pumuzi, simba athani kama amekufa. Nyama akaja, akamchia pua, lakini akiona kama mzoga tu akamwacha. Simba alipokwisha kwenda zake wala hakuna tena hatari, mtu yule akashuka katika mti akacheka akamwambia mwensiwe, "Neno gani ulilokwambia simba alipotia kanwa sikioni pako?" Mwenzake akamwambia, "Ndilo hili, mwangalie sana ayari yule alioko mtini, wala usimwamini tena."

KILIO CHA NGUUWE.

MTU mwerevu sana amepata kuweza kulia kama nguuwe, hatta watu wote wakathani mdipo nguuwe, lakini hako. Mtu mkulima akamwambia kama yeye atampita. Wakaja wote wawili, yule mwerevu akalia watu wote wakamisifu sana. Mkulima akaleta nguuwe ameficha nguo ni mwake hatta kwa zamu yake akamfanya, akalia. Watu wakamkaripia, wakamnena mjinga, wakasema, "Hii si santi ya nguuwe." Akazifunua nguo zake, wakamwona ndiye nguuwe aliyelia.

FARASI NA PUNDA.

FARASI mzuri alitoka bandani mwake, akapiga mbio njiani akilia. Akaona punda mwenyi mzigo, akamwambia kwa maneno ya kiburi, "Similla! similla upesi, nisikupige teke." Punda akanyamaa akajitenga njiani. Baadaye frasi akaenda palipo vita, alikuwa akimchukua bwana wake, akapata kupigwa, jicho likapofuka, hatta aliporudi akatiwa kazini. Punda akamkuta akasema, "Je! kiburi chako kimepoteaje, hali yako ya leo thaifu kuliko yangu."

NJIWA NA PANYA.

MTU mtega ndege aliuficha wavu katika majani. Akatupa juu yake mtama mwingi. Njiwa wakaja wakauona mtama. Mfalme wao akawaambia, "Ngojeni, ni nani aliyeutupa mtama huu, tufanye shauri kwanza." Njiwa hawakumsikiliza wakashuka wote, miguu yao ikashikwa na wavu, wakasema, "Tumekufa." Mfalme wao akawaambia, "Mbona hamkunisia? Bassi insikate tamaa, jaribu wote pamoja karuka juu, labuda mtatoka." Wakaruka wote pamoja wakauinua wavu wakaenda zao. Wa-

kasema, "Tufanyeje sasa, hatuwezi kuvuta miguuu katika wavu." Mfalme wao akawaambia, "Twenende kwa Mfalme wa panya, labuda yeye atatusayidia." Wakenda, hatta, walipofika, wakamwona mfalme wa panya akikaa kitako barazani mwake. Wakamwambia, "Tumejua kukuomba utusayidie, tumeshikwa na wavu huu." Mfalme wa panya akawaambia asikari zake, wakatafunu wavu, nao njiwa wakatoka marra. Wakamwambia panya, "Ndinyi rafiki kwa matendo, wala si kwa maneno tu." Wakaruka, wakaenda zao.

JOGOO NA ALMASI.

JOGOO alitoka alfajiri mapeina, akawika marra nyingi. Tena akapekuapekua akitafuta chakula. Akaona almasi nzuri sana. Akaitazama akaitupia mbali, akisema, "Chafaa nini kitu hiki kizuri? Punje moja ya mtama imekipita marra elfu."

MFUKO WA FETHA.

WATU wawili walikuwa wakisafiri pamoja, wakapatana washarikiane katika mambo yote ya njiani. Hatta walipokwisha kufika nusu ya njia, mmoja wao akaona mfuko wa fetha.

Akasema, "Nina baketi leo, nimepata fetha nyingi, mitanunua frasi, nisiende tena kwa migun." Mwenzake akamwambia, "Hاتuku-patana kusharikiana katika mambo yote." Akamwambia, "Je! Sikunona mimi peke yangu? Sisharikiani na mtu." Marra wakasikia wata wakija mbio, wakipiga kelele, "Weki! Wevi!" Yule alionuna mfuko wa fetha akasema, "Twende tujifiche, wasipate kutukumata, labuda watatuua." Mwenzake akamwambia, "Je! Hukouona peke yako? Husharikiani na mtu katika fayida, wala mimi siharikiani nawe katika kupigwa."

MBWA WA MWITU NA MWANA KONDODA.

SIKU moja mbwa wa mwitu alikuja anywe katika kijito cha maji, akamkuta mwana kondoo mchanga akisimama karibu na kijito. Mbwa wa mwitu akataka kugombana naye apate kumua. Akamwambia, "Mbona unaburugaboruga matope nisipate maji safi?" Kondeo mchanga akamwambia, "Ginsi gani nikutilietaka majini, yakiwa yanashuka kwako kwanilia mimi?" Mbwa wa mwiba aka-

mwambia, "Uthubutuje kunywa wewe, kabla sijanywa mimi?" Akamwambia mwana kudoo, "Mimi sinywi maji, maziwa ya mamangu yanitosha." "Bassi," akamwambia mbwa wa mwitu, "mbaya wee, mwaka jana umenitukana." "Ee Bwana," akamwambia mwana kondoo, "mwaka jana nalikuwa sijazaliwa." Mbwa wa mwitu akakasirika sana akamwambia, "Kama si wewe, ndiye baba yako, sijui kuwapambanua, mimestahili kufa wote." Akamkamata, akamuə, akamla.

IMBU NA NG'OMBE.

HAPO kale imbu alikaa kitako katika pembe lake ng'ombe, akamwambia, nimekaa kitako pembeni mwako ukiniona mzito mno uniambie niende zangu." Ng'ombe akamwambia, "Singalijua uliko, usiponiambia." Akapunga kitwa akamdaka imbu kwa ulimi.

MWANA MBUZI NA MBWA WA MWITU.

MWANA mbuzi aliyepotea alimwona mbwa wa mwitu, akataka kukimbia asiweze. Akiona

kama hana buddi kufa, akamwambia mbwa wa mwitu, "Yakini, bwana utanichinja, illa tafathali nicheze kwanza upate kucheka, ukipiga mzomari nitakufanyia mchezo mzuri sana." Mbwa wa mwitu akapiga mzomari, mwana mbuzi akarukaruka akacheza sana. Hatta watu waliokuwa wakipita wakasikia sauti ya mzomari wakaja kutazaina. Mbwa wa mwitu akiwaona akakimbia. Mwana mbuzi akarudi kwa ke wala tangu siku ile hakuwaacha wenzake.

PAKA ASIYE NA MKIA.

PAKA aliyekwenda akamate kuku akansawa na mtego, akapata kuokoka, illa mkia wake akakatika na mtego. Alipofika kwake akaona killa paka akimtzama hucheka kwa sababu hana mkia. Bassi walipokusanyika paka wote wafanye shauri, yule akasimania akawambia, "Nina neno moja, mikia yetu inatutaa-bisha sana, tukitaka kujificha tunduni mkia hutoka, tukienda hatuna buddi kuuvuta nyuma ao kuupandisha juu, hatuwezi kuuficha, hatta tukiona panya tunaupigapiga mkia, naye hutusikia hukimbia, marra kwa marra tumenaswa kwa mkia mtegoni. Mimi naona afathali tuji-

kate wote mkia tusitaabike tēna nao.” Paka mzee akamwambia “Tangu lini umeona mkia ndio taabu, nathani, tangu ulipokupotea tu.”

MWEMBE NA 'MWANZI.

MWEMBE ulioko karibu na mto uling'oka kwa tufanu, ukaanguka mtoni. Tufanu ilipokwisha akaona 'mwanzi unasimama wala haukuthuruliwa. Akauambia, “Ginsi gani wewe uliye thaifu umeokoka na mimi niwenyi nguvu nimepotea ?” 'Mwanzi akamwambia, “Kwa sababu ya kiburi chako, mimi nikisikia upepo marra nikainama, wewe hukukubali kuinama, ukavunjika.”

VYURA NA MAFAHALI.

VYURA vilivyoko karibu na ziwa wakaona mafahali wawili wakipigana. Akasema chura kimoja, “Tazama, Tazama, tufanyeje.” Chura kijana akamwambia, “Usiogope. hawa ng'o-mbe, si kama sisi, hawapigani na vyura. “Kwelli,” akamwambia chura mzee, “lakini wakipita hapa watakanyaga juu yetu, watatuua wasipotukumbuka.”

MBWA WA MWITU SAMAWATI.

MBWA wa mwitu akiingia mjini usiku aka-tumbukia katika pipa la rangi ya samawati, assubui akija mwenyi rangi akamthania ame-kufa, akamtoa akamtupa njiani. Mbwa wa mwitu akijiona salama akakimbia mwituni. Nyama za mwituni wakamwona wakataajabu wakiona rangi yake nzuri. Akiwasikia waki-msifu akawaambia, "Mimi si kama ninyi, mi-mi mfalme wa mwituni." Wakaja wote wakamleshimu. Halafu nyama wakaona namna yake na desturi zake kama za mbwa wa mwitu, wakawaambia, "Si huyu mmoja wenu?" Mbwa wa mwitu wakawaambia, "Twamwona rangi yake mbali, lakini namna yake kama yetu. Usiku huu tutamjaribu kama ndiye mmoja wetu." Hatta usiku mbwa wa mwitu wakamfuata wakamzungaka, wakapiga kelele wakalia sana, wala ye ye hakuweza kujuzuia akalia pamoja nao. Nyama wote wakisikia wakache-ka, wakamwambia, "Tumekujuua sasa, ndiwo mbwa wa mwitu, wala si mfalme wetu."

MTU NA KIJANA NA PUNDA.

MTU na mtoto wake walikuwa wakimleta

punda injini wapate kuza. Wakienda wakakuta vijitna waunawake wakiteka maji wakawa-chekelea, wakisema, "Tazama wajinga hawa, punda hana wzigo, naø hawajui kumpanda." Mtu akiwasikia akamweka kijana juu ya punda. Wakiendelea mbele wakapita waliopo wazee wamekaa kitako. Mzee mmoja akasema, "Tazama kama nilivyokuwa nikisema, siku hizi vi-jana huwatharau wazee. Kijana amepanda punda, tabaye anakwenda kwa miguu." Mtu alipomsikia akapanda punda mwenyewe, kijana akashuka. Baadaye watu wangine walipopita wakamwambia, "Je Baba! mbona unamwacha mtoto aende kwa miguu, huoni kama amechoka, hawezi kwenda kama punda wako." Mtu akiwasikia akampandisha kijana nyuma yake. Wakawa wamefika karibu na mji walipokutana na mtu, akawaambia, "Punda huyu ndiye mali yenu?" Wakamwambia, "Mali yetu." Akawaambia, "Nalithani ndiye mali ya watu mliomkwiba. Mtamfisha marra, hn-wezi kuwachukua watu wawili. Afathali mmchukue ninyi." Mtu akasema, "Bass tu-jaribu." Wakamfunga miguu wakamchukua mpikomi. Hatta walipofika mtoni watu wa

njiani wakacheka wakapiga kelele, punda aka-on-a khofu'akapiga teke akaanguka mtoni aka-tota. Mtu na kijana wakarudi kwao wakiambiana, "Tumejaribu kuwapendeza wote, wala hatukumpendeza mtu."

MTU NA PESA.

MTOTOTO aliona pesa za watu pasipo mtu, aka-twaa moja akamletea mamaye. Akaitwaa akaampa'kidogo'sukari. Marra kwa marra akatwaa vitu vidogo hatta akawa mwivi akawa tena mtu mbaya kabisa. Mwisho akahukumiwa auawe. Walipokuwa tayari wamue akaona mamaye akisimama karibu akalia. Akawaambia asikari, "Ngojeni, niinbusu mamangu." Mama wake ukuju, akamkumbatia, akamuma sikio lake. Watu waliopo wakachukizwa sana, wakasema, "Haikutoshi kufa kwa sababu ya uovu wako usipomumiza mama yako?" Akawaambia, "Yee ndiye asili ya uovu wangu wote, kama angalini-piga nilipoanza kwiba singalikufa leo."

KUKU NA MAFARANGA.

KUKU alikuwa na mafaranga akatembea a-kiwatafutia chakula. Akiwa karibu na kisima

faranga nimoja akaruka ukingoni akatumbu-kia. Kuku akasikitika sana. Hatta alipomwona mtoto wake wa zamani amekuwa jogoo, akamwambia, "Mwanangu usende kisimani, usife na wewe." Jogoo akathani, "Mbona nisende kisimani, labuda ameficha humo chakula." A-kaenda akatazama chini sana, akaona kama jogoo mgine yuko chirii, akawika akatazama akamwona tena, akaruka chini apate kumfukuzza, akazama majini, akafa.

UDONGO NA WARIDI.

MTU akiokota udongo akauona unanuka vema sana, akasema, "Je! umepataje kunuka hi-vi?" Udongo ukamwambia, "Nimekaa siku nydingi karibu na waridi, wala sina buddi kunuka vema."

MBWA WA MWITU NA KORONGO.

MBWA wa mwitu akitembea katika nyama akapigwa na mshale akajiona anakufa. Akaona korongo akamwambia. "Nakuomba uniletée maji ya kunywa nipate nguvu za kutafuta chakula." Korongo akamwambia, "Nikikuletea maji, utanila mimi, bassi sileti, kua heri."

PUNDA NA CHUMVI.

MTU alikwenda na punda kununua chumvi. Walipokuwa wakirudi punda akaona mzigo wake mzito. Hatta akipita mtoni akaanguka, chumvi kikayeyuka, punda akaona mzigo ume-kuwa mwepesi. Akafurahi sana na walipokwenda marra ya pili akaanguka makusudi kuko huko, chumvi kikapotea. Mwenyewe akiona busara ya punda, hanunui tena chumvi, akale-ta mchanga tu. Puuda akaanguka mtoni, mchanga ukapata maji, hatta alipotoka akaona mzigo wake umezidi sana kuwa mzito akatubu.

MBWA WA MWITU NA MBWA WA MJINI.

MBWA wa mwitu aliokonda sana akamwona mbwa wa mjini mnono na mzima, akamwuliza, “Ginsi gani, wewe umenona sana, mimi siwezi kupata chakula?” Mbwa akamwambia, “Kiko kwangu chakula tele, kazi yangu ku-wafuknza waivi, bwana wangu ananipenda sana, ukifuatana nami nitakupatia chakula.” Walipokuwa wakienda, mbwa wa mwitu aka-na alama shingoni mwa mbwa wa mjini, aka-

mwuliza, "Alama gani hii nionayo shingoni mwako?" Akamwambia, "Lnbuda ya mkufu wangu." Akamwambia, "Mkufu gani?" Akamwambia, "Wakinitaka nisiwefukuze watu watifunga pahali pangu, nao waniletea nyama na maji na chakula kizuri." Akamwambia mbwa wa mwitu, "Bassi, mwenzangu, kua heri, napenda sana chakula, lakini kutiwa mkufu sioni vema kabisa."

MTU NA SIMBA NA SUNGURA.

MTU alitaka kumtega sungura, akachimba shimo akalifunika na miti midogo na majani, akatia chambo katikati. Sungura akaja akaona kama labuda hila ya watu, wala hakuthubutu kwenda karibu sana. Baadaye simba akaja akaenda marra kikitwaa chambo akaanguka shimonii. Mtu akija akaona miti imepomoka akashuka amue sungura, akauawa mwenyewe na simba.

MKULIMA NA PAA.

WATU walipokuwa wakiwinda nyama, paa akamjia mkulima akataka ruksa ajifiche kijumbani mwake. Mkulima akamwahidi asimtoe.

Watū walipoūka wakamwaliza mkalima, “ U-meona nyama wakipita hapa ? ” Akamwambia, “ Sikuona,” lakini kwa kidole akawaonyesha kijumba chake, akathani, “ Akinisikia paa ataka-kaa kitako hatta watakapokaribia.” Lakini wa-winda nyama walipita njia nyigine, paa aka-toka akaenda zake. Mkuuina akawambia, “ Huna shukrani, hukusikia nilivy-kesetiri ? ” Paa akamwambia, “ Kweli umenisetiri kwa neno lakini kwa mkuono umenitoa, sikuamini tem.”

KUNGURU NA SUNGURA.

KUNGURU alikaa intini mwenyi midomoni kipande kizuri cha nyama. Sungura akamwona akataka sana kuipata nyama. Akamwambia, “ Saablkheiri bwana wangu.” Kunguru aka-nyamaa kimya. Sungura akamwambia, “ Ndiwe ndege nzuri, sikuona kabisa nyama mzuri kama wewe.” Kunguru akapendezewa, lakini halifunui kanwa. Sungura akamwambia, “ Naena santi yako nzuri sana, nitakaa furahani inchala kuchwa nikikusikia ukiumba, usikatae nakuoniba, unifurahishe intumwa wako ? ” Kunguru akayasikia waneno yake mazuri, akafunua ka-

nwa atoe sauti, nyama ikaanguka, sungura akaikamata akaenda zake mbio, wala hakukawia asikilize.

PUNDA NA PAKA NA JOGOO.

PANYA kijana aliouka' kuteebce ak ndi
mbio kwa inamaye akomwambia, "Nimeoma
nyama mkali sanaa akaniogofya neno. Atakwe-
nda kwa migai miwili anachukuo bandera nye-
kundu juu ya kivu anapigapiga nibavum kwa
nikono. Hatta akiniona minni akafunus kauwa
kubwa akalia soma, nikathania atanila merra,
nikakimbia. Bassi kama hangaliniogofya ninga
lipata kuzungumiza na nyare uzuri sana, ndiye
mwenyi nyele nyororo sana na macho makubwa,
na takia mrefu, akaupanga takia akanitazama
sana, naavi ningalitoa salamu aliyekuwa nyame
yule mkali akamifukuza." Matayye akaewa
mbia, "Nimeefutahiwa sana njikikoma salamu,
yule nyama aliyelia hangekuu uro, ndiye jogoo
wala hatumwogopi, lakinai yalo va pili twanwo-
gopa mao ndiye paka uela punya, na kama
ungalikujwa angalikujla wewe."

MSUFI

SIKU moja watu wawili walikuwa wamejinyosha chini ya msufi kwa sababu juu kali. Wakatazama juu, mmoja wao akasema, "Msufi hauzai matunda." Mwenzake akajibu, "Kweli zati kama huu haufai neno." Msufi akamwambia, "Ginsi gani sifai neno, mbona mmejinyosha haku, illa niwatie kivuli? Nimewaborodisha ninyi, nanyi mnaseina sifai neno."

MBWA ALIYESONGWA.

KONDOO mmoja alikuta mwenzake akata-ka habari. Akamwambia, "Mbwa wetu ame-songwa leo. Jana alikula mwana kondoo mchanga, akamna mama yake akamoma mchunga." Akamwambia, "Nalithani mbwa wenu, mbwa mwema sana. Amepataje kufanya mambu haya?" Akamwambia, "Tumemulizm, akasema, tangu miaka kumi sikukosa, illa jana usiku nalimwona mbwa wa mwitu amechukua kondoo mchanga, nikamfuata, nikamfukuza nikaona mtoto wa kondoo amekufa, wala sikuweza kujizua nikaanza kumla. Akaja mama yake, nikathani, huyu atanishtaki, nikamshika

akapiga yowe, nikaona sina buddi kumua. Lakini mchunga amemsikia akaja akataka kunipiga, nikumua. Bassi sasa watanisonga, kama ningalijizuia kwanza, singalikosa.”

NDEGE NA NYAMA NA POPO.

ZAMANI za kale ndege walipigana na nyama. Kwanza nyama zalishinda, popo akaja akasema, “ Mimi nyama, wala si ndege, tazama meno yangu na masikio, ndege hazinayo meno na masikio.” Baadaye ndege zikawashinda nyama. Popo akasema, “ Mimi ndege, wala si nyama, nyama hawezi kuruka.” Halafu ndege na nyama wakapatana, popo akafukuzwa nao wote, hatta leo hujificha paangoni na tunduni, wala hatoki illa usiku asipoonekana sana.

TUMBILI NA CHUPA.

TUMBILI aliona chupa lenyi sukari, akaingiza mkono akashika konzi, wala hakuweza kuondoa mkono. Akajaribu sana hatta angalikamatwa na mwenyi chupa, kama hangalimwona sungura. Sungura akamwambia, “ Mnitolee mimi kwanza sukari chache, nitakwambia ginsi utaka-

vyookoka;" Tumbili akaliacha konzi la kwanza akatwan sukari chache vidoleni, akaona anaweza kuongoa mkono. Sungura akamwambia, " Msiwe na choyo, twaa kidego tu, na utapata yote."

FRASI NA MBWA WA MWITU NA SUNGURA.

SUNGURA alikuwa akitembea akitaka chakula asipate. Akakuta mbwa wa mwitu, akamwambia "Tazama frasi yule, ukinisayidia labuda utaweweza kumua." Wakaenda wote hatta walipofika, wakainwona mkubwa sana, sungura akamwambia, "Jina lako nani, na bwana wako anakwitwaje?" Frasi akamwambia, "Jina langu fullani, na jina la bwana wangu linaandikwa katika ukwato wangu wa nyuma usome wewe, mimi sijui kulitamka vema." Sungura akamwambia, "Mimi sijui kusoma, lakini mwenzangu ndiyé mwenyi elimu nyingi." Mbwa wa mwitu akapendezewa, akisifiwa na sangura akaenda kutazama, frasi akampiga teke akamua.

NDEGE NA MAKINDA YAKE.

NDEGE alikaa na makinda yake katika mpu-

nga hatta siku moja akirudi jioi, makinda yake wakamwambia, "Watu wawili wamekuja leo, mmoja wao akamwambia mwenziwe, Ee mwanangu, naona mpunga unawiva enenda kawaite marasiki yetu waje watusayidie tuvune." Makinda waksona hofu yingi. Mzee akamwambia, "Hapana hofu leo." Siku ya pili yake mtu akaja akamwambia mwanawewe, "Enenda kawaite jamaa zetu watusayidie." Ndege akamwambia makinda yake, "Bassi tustarebe, jamaa hawaji upesi kuwasayidia jamaa." Baada ya siku nitu akaja tena, akamwambia niwanawewe, "Uje kesho assubui mapema tuvune hapusisi." Ndege akipata habari akaseuna, "Tende zetu sasa, intu akiteunda kazi mwenyewe hutendeka."

MTU NA SAMAKI.

MTU alikwenda kavua samaki akamtwaa mmoja naye mdogo. Samaki akamwambia, "Unirudishe majini nipate kukua, sasa ni mdogo mno, halafu ukinivua nitakufaa sana." Mvungi akamwambia, "Labuda, lakini sasa ni mekupata, labuda nkiwa mkubwa sitakupata tena, afathali nisikuache."

NG'OMBE NA NDAMA.

ZAMANI za kale ndama, aliokuwako karibu na Rumi, alimwambia ng'ombe aliokuwako katika kazi ya kulima, "Ewe mtumwa myo-nge wee, tazama mimi, sina illa kuchenza tu." Ng'ombe akamtazama, wala hakusema neno. Baada ya siku tatu watu wa Rumi wakafanya karamu kubwa. Ng'ombe akastarehe wala hakuenda kazini, akaona watu wakaja, waka-mchukua ndama wamchinje, akasema, "Kama huu ndio mwisho wa kuchenza, afathali nisiache kutenda kazi."

MBWA WA MWITU NA KONDOO.

PALIKUWA vita siku nyingi katika kondoo na mbwa wa mwitu. Baadaye mbwa wa mwitu wakawaambia kondoo, "Mbwa zenu ndio sababu ya vita, wanatulilia sikuzote, wala ha-watuachi tuje tupatane nanyi. Bassi ukiwa-cha mbwa waende zao tutapatana nanyi, na tu-tawapa ninyi watoto wetu kwa amana." Kondoo wakakubali, wakawaacha mbwa waende zao, wakawapokea watoto. Hatta usiku watoto wa **mbwa wa mwitu** wakalia, wazee wao wakaja,

wakasema, “Mbona unawaonea watoto wetu, walie hivi? Mmevunja mapataco.” Wakaja wakawakamata kondoo wakawaua, wala hakuna wa kuwasayidia.

MWANA MBUZI NA MBWA WA MWITU.

MWANA mbuzi aliokuwa juu ya nyumba asipopatikana, akamwona mbwa wa mwitu akipita, akamchokoza akamtukana. Mbwa wa mwitu akamwambia, “Nakusikia, husemi maneno haya illa kwa sababu ya kuwa huko juu.”

JOGOO NA SUNGURA NA MTEGO.

SUNGURA akitafuta chakula, akaingia wali po kuku akataka kuwakamata, illa akiwatazama kuku akanaswa na mtego. Jogoo akamwona hawezi kwenda, akaja amtazame. Sungura akamwambia, “Ee rafiki, nimepata hasara kwa sababu yako. Nalikuwa nikirudi kwangu, nikaona sina buddi kukutolea salaamu, bassi nikiingia nimenaswa, tafathali uniletee kisu nikate tanzi hili.” Jogoo akaenda akamwa-

PUNDA NA CHUMVI.

MTU alikwenda na punda kunnua chumvi. Walipokuwa wakirudi punda akaona mzigo wake mzito. Hatta akipita mtoni akaanguka, chumvi kikayeyuka, punda akaona mzigo ume-kuwa mwepesi. Akafurahi sana na walipokwenda marra ya pili akaanguka makusudi kuko huko, chumvi kikapotea. Mwenyewe akiona busara ya punda, hanunui tena chumvi, akale-ta mchanga tu. Punda akaanguka mtoni, mchanga ukapata maji, hatta alipotoka akaona mzigo wake umezidi sana kuwa mzito akatibu.

MBWA WA MWITU NA MBWA WA MJINI.

MBWA wa mwitu aliokonda sana akamwona mbwa wa mjini mnono na mzima, akamwuliza, “Ginsi gani, wewe umenona sana, mimi siwezi kupata chakula?” Mbwa akamwambia, “Kiko kwangu chakula tele, kazi yangu ku-wafukuza waivi, bwana wangu ananipenda sana, ukifuatana nami nitakupatia chakula.” Walipokuwa wakienda, mbwa wa mwitu akao-na alama shingoni mwa mbwa wa mjini, aka-

mwuliza, "Alama gani hii nionayo shingoni mwako?" Akamwambia, "Labuda ya mkufu wangu." Akamwambia, "Mkufu gani?" Akamwambia, "Wakinitaka nisiwafukuze watu wanifunga pahali pangu, nao wanilettea nyama na maji na chakula kizuri." Akamwambia mbwa wa mwitu, "Bassi, mwenzangu, kua heri, napenda sana chakula, lakini kutiwa mkufu sioni vema kabisa."

MTU NA SIMBA NA SUNGURA.

MTU alitaka kumtega sungura, akachimba shimo akalifunika na miti midogo na majani, akatia chambo katikati. Sungura akaja akaona kama labuda hila ya watu, wala hakuthubutu kwenda karibu sana. Baadaye simba akaja akaenda marra kukitwaa chambo akaanguka shimonii. Mtu akija akaona miti imepomoka akashuka amue sungura, akauawa mwenyewe na simba.

MKULIMA NA PAA.

WATU walipokuwa wakiwinda nyama, pa a kamjia mkulima akataka ruksa ajifiche kijumbani mwake. Mkulima akamwahidi asimtoe.

Watu walipouka wakamwaliza mkulima, "U-meona nyama wakipita hapa?" Akamwambia, "Sikuona," lakini kwa kidole akawaonyesha kijumba chake, akathani, "Akinisikia paa ataka kitako hatta watakapokaribia." Lakini wawinda nyama walipita njia nyingine, paa atakota akaenda zake. Mkulima akamwambia, "Huna shukranji, hukusikia nilivyokasetiri?" Paa akamwambia, "Kweli umenisetiri kwa meno lakini kwa mkono umenitoa, sikuamini teni."

KUNGURU NA SUNGURA.

KUNGURU alikaa intini mwenyi midomoni kipande kizuri cha nyama. Sungura akamwona akataka sana kuipata nyama. Akamwambia, "Saablkheiri bwana wangu." Kunguru akanyamaa kimya. Sungura akamwambia, "Ndiwe ndege mzuri, sikuona kabisa nyama mzuri kama wewe." Kunguru akapendezewa, lakini halifunni kanwa. Sungure akamwambia, "Naena sauti yako mzuri sana, nitakaa furabani nichala kuchwa nikikusikia ukiinuba, usikatae nakuo-mba, uufurahishe intumwa wako?" Kunguru akayasikia maneno yake mazuri, akafunua ka-

nwa atoe sauti, nyama ikaanguka, sungura akaikumata akaendza zake mbio, wala hakukawia asikilize.

PUNDA NA PAKA NA JOGOO.

PANYA kijama olitoka' kitembea akundi mbio kwa mamaye akamwambia, "Nimeona nyama mikali sana akaniogofya inio. Anakwendza kwa mingau miwili anachukua bandera nye-kundu jnu ya kitwe anapigapiga nibavum kwa mikono. Hatta akiniona nini akafunus kanwa kabwa akalia sana, nikathania atanila marra, nikakimbia. Bassi kama hangaliniogofya ninga lipata kuzungumza ba nyama mzuri sana, ndiye mwenyi nyele nyororo sana na macho makubwa, na takia oreeru, akanpunga takia okanitazama sana, naavi ntingalitoa salatua, alipokuja nyama yule mikali akanifukuza." Mamaye akamwambia, "Nimefurathiwa sana rjikitunga salatua, yule nyama ahyelia hangekuturu, ndiye jogoo wala hatuniwogopi, lakini yalo wa pili twamwogopa mao ndiye paka mla panya, na kama ungalikawja angalikida wewe."

MSUFI

SIKU moja watu wawili walikuwa wamejinyosha chini ya msufi kwa sababu juu kali. Wakatazama juu, mmoja wao akasema, “Msufi hauzai matunda.” Mwenzake akajibu, “Kweli mti kama huu haufai neno.” Msufi akamwambia, “Ginsi gani sifai neno, mbona mmejinyosha huku, illa niwatie kivuli? Nimewaburadisha ninyi, nanyi mnaseina sifai neno.”

MBWA ALIYESONGWA.

KONDODO mmoja alikuta mwenzake akataka habari. Akamwambia, “Mbwa wetu amesongwa leo. Jana alikula mwana kondoo mchanga, akamna mama yake akamuma mchunga.” Akamwambia, “Nalithani mbwa wenu, mbwa mwema sana. Amepataje kufanya mambu haya?” Akamwambia, “Tumemuliza, akasema, tangu miaka kumi sikukosa, illa jana usiku nalimwona mbwa wa mwitu amechukua kondoo mchanga, nikamfuata, nikamfukuza nikaona mtoto wa kondoo amekufa, wala sikuweza kujuizia nikaanza kumla. Akaja mama *yake, nikathani, huyu atanishtaki, nikamshika*

akapiga yowe, nikaona sina buddi kumua. Lakini mchunga amemsikia akaja akataka kunipiga, nikamura. Bassi sasa watanisonga, kama ningalijizuia kwanza, singalikosa.”

NDEGE NA NYAMA NA POPO.

ZAMANI za kale ndege walipigana na nyama. Kwanza nyama zalishinda, popo akaja akasema, “ Mimi nyama, wala si ndege, tazama meno yangu na masikio, ndege hazinayo meno na masikio.” Baadaye ndege zikawashinda nyama. Popo akasema, “ Mimi ndege, wala si nyama, nyama hawezi kuruka.” Halafu ndege na nyama wakapatana, popo akafukuzwa nao wote, hatta leo hujificha paangoni na tunduni, wala hatoki illa usiku asipoonekana sana.

TUMBILI NA CHUPA.

TUMBILI aliona chupa lenyi sukari, akaingiza mkono akashika konzi, wala hakuweza kuondoa mkono. Akajaribu sana hatta angalikamatwa na mwenyi chupa, kama hangalimwona sungura. Sungura akamwambia, “ Mnitolee mimi kwanza sukari chache, nitakwambia ginsi utaka-

vyookoka," Tumbili akaliacha konzi la **kwanza** akatwaan sakari chache vidoleni, akaona anaweza kuongoa mkono. Sungura akamwambia, " Msiwe na choyo, twaa kidogo tu, na utapata yote."

FRASI NA MBWA WA MWITU NA SUNGURA.

SUNGURA alikuwa akitembea akitaka chakula usipate. Akakuta mbwa wa mwitu, akamwambia "Tazama frasi yule, ukinisayidia labuda intawenza kumua." Wakaenda wote hatta walipofika, wakainwona mkubwa sana, sungura akamwambia, "Jina lako nani, na bwana wako anakwitwaje?" Frasi akamwambia, "Jina langu fullani, na jina la bwana wangu linaandikwa katika ukwato wangu wa nyuma nsome wewe, mimi sijui kulitamka vema." Sungura akamwambia, "Mimi sijui kusoma, lakini mwenzangu ndiyé mwenyi elimu nyingi." Mbwa wa mwitu akapendezewa, akisifiwa na sungura akaenda kutazama, frasi akampiga teke akamua.

NDEGE NA MAKINDA YAKE.

NDEGE alikaa na makinda yake katika mpu-

nga hatta siku moja akirudi jioni, makinda yake wakamwambia, "Watu wawili wamekuja leo, mmoja wa o akamwambia mwensiwe, Ee mwauangu, naona mputiga uniwiva enenda kawaite marafiki yete waje watusayidie tenuvune." Makinda wakaona hofu yingi. Mzee akamwambia, "Hepana hofu leo." Siku ya pili yake mtu akaja akamwambia mwanawewe, "Enenda kawaite jamaa zetu watusayidie." Ndege akamwambia makinda yake, "Bassi tustarebe, jamaa hawaji upesi kuwasayidia jamaa." Baada ya siku mtu akaja tena, akamwambia mwanawewe, "Uje keslio assubui mapema tuvune hapa sisi." Ndege akipata habari akasema, "Tende zetu sasa, intu akitenda kazi mwenyewe hutendeka."

MTU NA SAMAKI.

MTU alikwendwa kuvua semaki akamtwaa mmoja naye ndego. Samaki akamwambia, "Unirudishe majini nipate kakoni, sasa ni indogo mno, halafu ukinivua nitakufaa sana." Mvungi akamwambia, "Labuda, lakini sasa ni mekupata, labuda ukiwa mkubwa sitakupata tena, afathali nisikuache."

NG'OMBE NA NDAMA.

ZAMANI za kale ndama, aliokuwako karibu na Rumi, alimwambia ng'ombe aliokuwako katika kazi ya kulima, "Ewe mtumwa mnyonge wee, tazama mimi, sina illa kucheza tu." Ng'ombe akamtazama, wala hakusema neno. Baada ya siku tatu watu wa Rumi wakafanya karamu kubwa. Ng'ombe akastarehe wala hakuenda kazini, akaona watu wakaja, wakamchukua ndama wamchinje, akasema, "Kama huu ndio mwisho wa kucheza, afathali nisiache kutenda kazi."

MBWA WA MWITU NA KONDOO.

PALIKUWA vita siku nyingi katika kondoo na mbwa wa mwitu. Baadaye mbwa wa mwitu wakawaambia kondoo, "Mbwa zenu ndio sababu ya vita, wanatulilia sikuzote, wala hatwuachi tuje tupatane nanyi. Bassi ukiwaacha mbwa waende zao tutapatana nanyi, na tutawapa ninyi watoto wetu kwa amana." Kondoo wakakubali, wakawaacha mbwa waende zao, wakawapokea watoto. Hatta usiku watoto wa *mbwa wa mwitu* wakalia, wazee wao wakaja,

wakasema, “Mbona unawaonea watoto wetu, walie hivi? Mmevunja mapataro.” Wakaja wakawakamata kondoo wakawaua, wala hakuna wa kuwasayidia.

MWANA MBUZI NA MBWA WA MWITU.

MWANA mbuzi aliokuwa juu ya nyumba asipopatikana, akamwona mbwa wa mwitu akipita, akamchokoza akamtukana. Mbwa wa mwitu akamwambia, “Nakusikia, husemi maneno haya illa kwa sababu ya kuwa huko juu.”

JOGOO NA SUNGURA NA MTEGO.

SUNGURA akitafuta chakula, akaingia wali po kuku akataka kuwakamata, illa akiwatazama kuku akanaswa na mtego. Jogoo aka-mwona hawezi kwenda, akajamta zame. Sungura akamwambia, “Ee rafiki, nimepata hasara kwa sababu yako. Nalikuwa nikirudi kwangu, nikaona sina buddi kukutolea salaamu, bassi nikiingia nimenaswa, tafathali unilettee kisu nikate tanzi hili.” Jogoo akaenda akamwa-

PUNDA NA CHUMVI.

MTU alikwenda na punda kununua chumvi. Walipokuwa wakirudi punda akaona mzigo wake mzito. Hatta akipita mtoni akaanguka, chumvi kikayeyuka, punda akaona mzigo ume-kuwa mwelesi. Akafurahi sana na walipokwenda marra ya pili akaanguka makusudi kuko huko, chumvi kikapotea. Mwenyewe akiona busara ya punda, hanunui tena chumvi, akale-ta mchanga tu. Punda akaanguka mtoni, mchanga ukapata maji, hatta alipotoka akaona mzigo wake umezidi sana kuwa mzito akatubu.

MBWA WA MWITU NA MBWA WA MJINI.

MBWA wa mwitu aliokonda sana akamwona mbwa wa mjini mnono na mzima, akamwuliza, "Ginsi gani, wewe umenona sana, mimi siwezi kupata chakula?" Mbwa akamwambia, "Kiko kwangu chakula tele, kazi yangu ku-wafukuza waivi, bwana wangu ananipenda sana, ukifuatana nami nitakupatia chakula." Walipokuwa wakienda, mbwa wa mwitu akao-na alama shingoni mwa mbwa wa mjini, aka-

mwuliza, "Alama gani hii nionayo shingoni mwako?" Akamwambia, "Labuda ya mkufu wangu." Akamwambia, "Mkufu gani?" Akamwambia, "Wakinitaka nisiwafukuze watu wanifunga pahali pangu, nao waniletea nyama na maji na chakula kizuri." Akamwambia mbwa wa mwitu, "Bassi, mwenzangu, kua heri, napenda sana chakula, lakini kutiwa mkufu sioni vema kabisa."

MTU NA SIMBA NA SUNGURA.

MTU alitaka kumtega sungura, akachimba shimo akalifunika na miti midogo na majani, akatia chambo katikati. Sungura akaja akaona kama labuda hila ya watu, wala hakuthubutu kwenda karibu sana. Baadaye simba akaja akaenda marra kukitwaa chambo akaanguka shimonii. Mtu akija akaona miti imepomoka akashuka amue sungura, akauawa mwenyewe na simba.

MKULIMA NA PAA.

WATU walipokuwa wakiwinda nyama, paa akamjia mkulima akataka ruksa ajifiche kijumbani mwake. Mkulima akamwahidi asimtoe.

Watu walipouka wakamwaliza mkalima, "U-meona nyama wakipita hapa?" Akamwambia, "Sikuona," lakini kwa kidole akawaonyesha kijumba chake, akathani, "Akinisikia paa ataka kitako hatta watakapokaribia." Lakini wawinda nyama walipita njia nyingine, paa aka-toka akaenda zake. Mkulima akamwambia, "Huna shukrani, hukusikia nilivyokasetiri?" Paa akamwambia, "Kweli umenisetiri kwa neno lakini kwa mkono umenitoa, sikuamini teni."

KUNGURU NA SUNGURA.

KUNGURU alikaa intini mwenyi midomoni kipande kizuri cha nyama. Sungura akamwona akataka sana kuipata nyama. Akamwambia, "Saablkheiri bwana wangu." Kunguru aka-nyamaa kimya. Sungura akamwambia, "Ndiwe ndege mzuri, sikuona kabisa nyama mzuri kama wewe." Kunguru akapendezewa, lakini halifunni kauwa. Sungure akamwambia, "Naena suti yako nzuri sana, uitakaa furabani inchara kuchwa nikikusikia ukiimba, usikatae na kuo-mba, unfurahishe istumwa wako?" Kunguru akayasikia waneno yake mazuri, akafunua ka-

kaja kumwona na kumletea zawadi. Karibu yake palikuwa kondoo aliye karibu kufa wala mtu haendi kumsayidia. Kondoo akasema, “Ginsi gani hii, wote waenda kwa punda, wala mtu haji kwangu?” Sungura akamwambia, “Hujui sababu? Punda akiwashukuru sauti inasikiwa killa pahali, lakini sauti yako thaifu, wala mtu akikusayidia hapati kusifiwa na watu.”

SUNGURA KATIKA KISIMA.

SUNGURA alitumbukia kisimani akajizua kitambo kwa ukuta asizame majini. Mbwa wa mwitu akaja akamtazama. Sungura akamwambia, “Ee rafiki enende upesi, ute kamba nipaye kutoka.” Mbwa wa mwitu akasema, “Ee rafiki, nakuona katika hatari nyingi, nakusikitikia sana.” Sungura akasema, “Haya, enende upesi nitakufa.” Mbwa wa mwitu akamwambia, “Moyo wang'u unaona huzuni nyingi kwa sababu yako.” Sungura akamwambia, “Usitoe maneno mazuri unilettee kamba.” Mbwa wa mwitu akaenda zake, akasema kwa ndani, “Marra nyingi yule aumenipa maneno

matupa, sisu umenilipia fashii zake.²² Akamwaelia sungura atoue.

PAA KATIKA MAJANI.

WATU wakiwa wimawinda nyama wakarowoni paa. Paa akaenda imbo akajificha katika vijito. Wacu wakamtafuta, wasin.wone. Hatta paa akaona majani matamu karibu na kauwa lake, akatwaa meja akala. Akasikiliza wala hakusikta neno akatwaa m'jani mangine akawasahau wawienda, hatta iatu aliyekuwa annekawia karibu na vijito akaona kama nyama yuko. Akawaita wenzake, wakamkamata paa.

SUNGURA NA KORONGO.

SUNGURA aitoka kumefanya mzaha korongo akamwita kwa karamu. Korongo alipoknjaji akaona vyakula vizori, lakini viimetawanyiko katika sahani pana hatta hawezi kutwaa illa kidogo kidogo tu kwa nchi za midomo yake. Sungura akala upesi, akamwambia korongo, “Mbora unatwaa kidogo kidogo tu, hnomi vema vyakula livi.” Korongo akamwambia, “Vya-kula vema sana, nawe umenifanya heshima

nyingi, uje nakuomba kesho kwangu nikufanyie karatuu mimi." Sungura akakubali. Hatta alipofika kwa korongo amepika vyakula vema sana, lakini amevitia katika machupa. Aka-mkaribisha sungura, akatia midomo yake mirefu chopeni akola sana, wala sungura hawezি kupata chakula, ilia akaramba katika tundu la machupa. Korongo akamwambia, "Mbona huli, nimetaka kuknheshimia kama uliyyonifanya jana." Sungura akamwambia, "Kweli, umenapite sana."

BATA ALIYEZAA THAHABU.

MTU alikuwa na bata aliyezaa killa siku yayi la thahabu. Akamwambia mkewe, "Sipendi kungoja siku nyingi, killa siku yayi moja tu naona haba." Mkewe akamwambia, "Afathali tunue bata tataona thahabu yote ndani yake, tutaipata marra." Akamwambia, "Kweli, shauri lako jema sana." Akamua bata, aka-ntumbua, akamwona bata tu, wala thahabu hupano.

MBWA NA JOGOO NA PAKA.

MBWA na Jogoo wakisafiri pameja katika

mwitu wakaona usiku wakachagua pahali pa kula. Jogoo akaruka juu mtini, mbwa akalala katika mvungu. Hatta assubui jogoo akawika mapema. Paka akasikia, akaja kutaka kumla. Akimwona akamwambia, "Ee rafiki yangu ushuke tapate kuzumgumza." Jogoo akamwambia, "Vema, illa umwamushe kwanza mweanzangu anayelala katika mvungu." Paka akathani, "Mwenzake jogoo ndiye kuku." Akaenda kumwamushe, akakamatwa na mbwa.

MBWA KATIKA MAJANI.

MBWA amelala katika majani, akaja ng'ombe akataka kuyala. Mbwa akamlilia akatos meno, akataka kumuma. Ng'ombe akamwambia, "Wafaa nini wee, huwezi kuyala majani, wala huniachi mimi niyale."

KURUKA KATIKA RODI.

Mtu aliyekuwa amesafiri huwaambia watu, kama katika safari zake amefanya mambo makuu sana. Kwanza wakafurahiwa wakiona kama mtu wa kwao amewapita wagoni wote,

hatta halafu akazidi kujisifu wakaona maneno yake ndiyo uwongo. Siku moja akasema, "Watu wa Rodi wajua kuruka sana, lakini mimi nimewapita wote, nikishindana nao nali-ruka thiraa thelathini." Mtu mzee akamwambia, "Bassi ujithanie upo sasa[katika Rodi ukaruke, tukuone hapa, tupate kukusadiki." Msafiri akanya[naza, wala tangu siku ile hakujisifu kama kwanza.

MZEE NA MTABIBU.

MWANAMKE mzee alikuwa hawezi macho, akamwita mtabibu, akamwambia kama atampa fetha nyangi akimponyesha macho. Mtabibu akaja akaona pambo la nyumba zuri sana, naye bibi hawezi kuona, akachukua kidogo kidogo pambo lake, halafu akamponyesha bibi. Alipotaka fetha, aka'mweka siku kwa siku, hatta akamshtaki kwa kathi. Kathi akamwambia, "Huoni sasa, mbona hukumpa ujira wake?" Akamwambia, "Sioni, kwanza nyumbani mwangu kulikuwa pambo zuri hatta leo silioni kabisa. Akinifanya nilione pambo langu nitampa ujira wake."

MBWA NA MWIVI.

USIKU wa giza mwivi alikuja kwa nyumba ya mwenyewe apate kwiba mali zake. Mbwa akamwona akalia. Mwenyi nyumba akaondoka, akatazama asione kitu, akamwambia mbwa anyamaze, akalala. Mwivi akiona amelala akarudi akajaribu kuufungua mlango apate kuingia. Mbwa akalia sana. Mwenyi nyumba alipoondoka mwivi amejificha, naye asipoona kitu akasikia kimya, akakasirika na mbwa, akamnenea ukali, akalala. Mwivi akarudi, mbwa akalia, lakini mwenyi nyumba akamkaripia tu. Hatta assubui akaona kama mwivi ameingia akachukua vitu vingi. Akakumbuka ginsi alivyomfanyizia mbwa ukali, akasema, “**Mtu** akimtukana rafiki yake, adui zake huona furaha.”

YAYA NA MBWA WA MWITU.

MBWA wa mwitu akizunguka kutaka chakula akasikia kitoto analia, yaya akamwambia, “Nyamaza wee, nyamaza, usiponyamaza nitakutupa nje, mbwa wa mwitu akukamate.”

Akangoja akasema, “Nitampata labuda.”
Baadaye kitoto akanyamaza, yaya skamwambia,
 “Ee kipenzi changu, akiija mbwa wa mwitu
 tutampiga hatta kufa.” Mbwa wa mwitu aka-
 sema. “Hawa waana Adamu hawajui maana,
 marra husema mema marra husema mabaya,
 hatuwezi kuwasadiki kabisa.”

FRASI NA NYATI.

HAPO zamani frasi aligombana na nyati,
wakafanya vita, illa frasi akawa anaziogopa
 pembe za nyati. Akaenda kwa mwana Adamu,
 akamtaka amsayidie, mwana Adamu aka-
 panda juu ya frasi akafuata nyati akampiga,
 akamua. Frasi akamwambia, “Ahsanti, ume-
 nifanyia fathili kuu, bassi ushuke.” Mwana
 Adamu akamwambia, “Mimi sasa natsaka uni-
 sayidie mimi, shishuki illa kazi yangu yote
 itakapokwisha.” Wala hatta leo haknumwacha
 frasi.

KATHI NA MASIKINI.

Mtu mwenyi shamba dogo alikwenda siku
 moja kwa kathi akamwambia, “Habari za

leo nzito, ndizo kama fahali wangu amemua ng'ombe wako." Kathi akamwambia, "Bassi huna buddi kumua fahali, ni kulinipia hasara yangu." Masikini akamsifu akamwambia, "Nimekossi kwa neno moja tu, ng'ombe aliye-uawa ndiye wangu na fahali ni wako." Kathi akakasirika sana akasema, "Kama ndivyo sikupi neno, enda zako upesi, nisikupige kwa sababu ya kuniambia habari za uwongo."

SUNGURA NA PAKA.

SUNGURA alimkuta paka katika mahali pa-wazi, akamwambia, "Mimi ninazo hila nyingi, lakini wewe ukiwa katika hatari utafanyaje?" Paka akamwambia, "Nina hila moja tu, labuda itanitosha." Marra wakaja mbwa wa niwitu wengi, paka akapanda mtini, sungura akataka kukimbia lakini mbwa wakamkamata wakamua. Paka akasema, "Hila moja yatosha, ikiwa njema."

UPEPO NA JUA.

UPEPO na jua walikuwa wakigombana. Killa munoja akasema, "Mimi mwenyi nguvu

kuliko wewe." Wakamwona mtu akipita. Upepo akasema, "Mimi nitaondoa joho lake nkinipita katika kazi hii utanishinda." Jua akakubali, upepo ukavuma sana, ukalishika joho ukajaribu kuliondoa. Mtu akalishika joho kwa mikono miwili wala hakuliacha. Baadaye jua akachoma sana, akatoka hari sana akavua joho lake, akatafuta mahali palipo kivuli. Jua akasema, "Huoni kama kushawishi kumepita kutia nguvu?"

SUNGURA NA MBUZI.

SUNGURA alitumbukia kisimani wala hakuweza kutoka. Mbuzi akaja akitaka kunywa, akamwona sungura, akamwuliza, "Maji haya matamu." Sungura akamwambia, "Maji haya matamu sana, bwana, sikuyaona maji matamu kuliko haya, ushuke tu utapendezewa sana." Mbuzi akashuka, sungura akapanda juu yake, akaruka akatoka, akamwachcha mbuzi kisimani.

KORONGO NA MBWA WA MWITU.

MBWA wa mwitu alikuwa na mfupa ume-kwama kooni mwake, wala hakuweza kuu-

ondoa. Akawaaumbia nyama zote kama atampa fetha nyingi atakayeondoa mfupa. Akaja korongo akaingiza midomo yake mirefu akaundoa mfupa. Akataka fetha. Mbwa wa mwitu akamwambia, "Wataka nini tena, huna shukrani, umetia kitwa cbako kinwani mwangu, wala sikukuuma, bassi ukimbie nisitubu."

JOGOO NA SUNGURA.

JOGOO alikuwa akiwika juu ya ukuta, sungura akamwona akataka kumpata amle. Akamwambia, "Umesikia habari?" Akamwambia, "Habari gani?" Akamwambia, "Kama nyama zote wamepatana, wala hakuna vita tena. Nyama hamfukuzi nyama, wala nyama hamwogopi tena nyama." Jogoo akanyamaza akanyosha shingo kama akitazama kitu. Sungura akamwambia, "Unatazama nini?" Akamwambia, "Naona mbwa za kuwinda nyama zinakuja mbio." Sungura akamwambia, "Bassi naenda zangu, kua heri." Jogoo akamwambia, "Unaogopa nini, umenipa habari za kupatana nyama zote." Sungura akamwambia, "Kweli, lakini mbwa hizo labuda hawajapata habari."

NJIWA NA CHUNGU.

'SIKU moja chungu ameanguka mtoni aka-chukuliwa na maji. Njiwa akamwona aka-msikitikia, akamtupia jani la mti, akapanda juu ya jani akavuka. Baada ya siku akamwona mtu mwenyi bunduki ametaka kumpiga njiwa. Alipokuwa tayari kupiga bunduki, chungu akamuma mguu, akamkosa njiwa, akaokoka.

MWISHO.

